Maana ya Siasa

Shaikh 'Alee Hassan Al-Halabee

Asili: Fiqhul-Waaqi' baynan-Nadhariyyah wat-Tatbeeq (p. 28-37)

Baada ya kuyafahamu yale yaliyopita yenye kutokamana na misingi iliyo thubutu na kuyaelewa vyema, inakuwa ni jambo la wajibu kujua mas-ala ya Siyasa ambazo inawapasa walinganizi kuziandama na kuwaachia wengine kuwa ni kielelezo katika maisha yao.

Imepokewa kutoka kwa Abu Hurairah (Radhiallaahu 'anhu) yakwamba alisema: Mtume wa Mwenyezi Mungu (Sallallaahu 'alayhi wasallam) amesema: "Banu Israa'il walikuwa wakiongozwa na Mitume, kila mmojawapo alipokuwa akifa, mwengine alikuwa akichukuwa nafasi yake. Hatahivyo, hakuna tena Mtume baada yangu mimi, lakini kutakuja khulafaa' (ma-khalifa) ambao watakaokuwa wengi." Wakasema: "Watuachia maagizo gani sisi kuwahusu wao?" Akasema: "Tekelezeni ahadi ya utiifu kwa (atakaekuwa) wa kwanza, kisha wa kwanza, kisha muwape haki zao, kwani Mwenyezi Mungu atawauliza wao kuhusu walivyo watawala nyinyi."[1]

Kwahivyo, maana ya Siyasa kwa upande wa utaalamu wa kisheria ni: "Kuhami na kulinda mas-ala ya Ummah." Na hili ndilo jambo lililokuja kuthibitishwa na Uislamu – kwa Aayaat na Ahaadeeth, na kwa maamrisho na hukmu zake, na kwa maamrisho yake na misingi. Kwahivyo, maana ya Siyasa katika kuzifahamu hali za watu ni kuyatekeleza misingi iliyowekwa na isiyobadilika ya Qur'aan na Sunnah kulingana na mazingara na matukio mapya, bila ya kukosa mafanikio yoyote, wala ugomvi wa hila!

Na siyasa hii si kama zile siyasa zisizo na maana yoyote ambazo misingi yake yamewekwa na makafiri na wasioamini Mungu, wenye sifa za ujanja wa kichinichini na ufisadi!! Wala siyasa hii si kama siyasa za Machivellian, siyasa za Urongo, udanganyifu, njama na kufanyiana hila! Wala siyasa hii si kama siyasa za Wafalme [4], ambazo asli yake zimejengewa juu ya ujanja wa kuhadaa, kusema urongo na uzandiki! Bali siyasa hii ni: "Siyasa zilizotakasika na ubainifu wa ki-Utume, mambo ambayo viongozi na raiya wake hawawezi kuishi yakosekanapo hayo." [5] Amma kuikusudia siyasa hii katika maisha na hali yetu ya leo – kwa malengo ya kujua jinsi ya kupambana nayo – inaingia chini ya mojawapo ya jinsi mbili:

La kwanza, ni yale matukio mapya yaliyo wazi-wazi, ambayo – pamoja na kwamba dalili zake na ushahidi wake ni thaabit – hukmu za Mwenyezi Mungu Aliye Mtukufu zikawa wazi. Hivyo-basi, inakuwa hukmu yoyote inayoafikiana na hali ilivyo, inatekelezwa.

La pili, hayo matukio mapya, yaliyotarajiwa yakiwa juu ya misingi ya dhana tupu na kubahatisha. Inabidi huku kubahatisha kufanyiwe upelelezi kwa uangalifu sana, kwa sababu asli yake haikuegemezwa juu ya msingi wowote

[1] Hasan: Imepokewa na Ahmad (no.7899), Ibn Mâjah (no.4036) na wengineo.

ulio imara, wala haina tegemeo madhubuti. Ndio utaona masuali mengi ya siyasa za ki-leo na njia zao tafauti za kujidhihirisha hufuata nyayo za dhana kama hizo na kubahatisha, na zikajengwa juu ya misimamo hiyo.

Hatahivyo, hii haimaanishi kuwa twakataa kuchukuwa tahadhari na kuwa waangalifu na wasikivu. Na hapana shaka – baada ya yote haya – yakwamba: "Kulinda na kuhifadhi mas-ala ya Ummah huu kunahitaji manhaj (mfumo). Sasa Jee, kuna manhaj yoyote ipatikanayo isipokuwa Uislamu? Kwahivyo Uislamu ni siyasa (kulinda na kuhifadhi mas-ala ya Ummah huu) juu ya mfumo wa ki-Islamu," [6] na wala sio juu ya mfumo wa vyombo vya habari na magazeti!

Kuzinduka kwenye Ukweli wa Uhakika:

Na ni wajibu kufahamu kuhusu msingi wa shari'ah isiyobadilika – ambao utakaoleta uhakika wenye kufungua fahamu zetu na kutuamsha katika ukweli wa uhakika wa hali zetu zilivyo – nao ni: Yakwamba misiba yoyote iliyotupata, au itupatayo hivi sasa, au itakayotupata, basi ni kwa sababu ya yale yaliyotangulizwa na mikono yetu; na ni kwa sababu ya makosa yetu kuhusiana na utekelezaji wa wajibu wa Dini yetu. "Na misiba inayokupateni ni kwa sababu ya mikono yenu, na (juu ya Mwenyezi Mungu) ansamehe mengi." [7] Na: "Na mwenye kufanya dhambi, basi ameifanyia nafsi yake (uovu)."

Kwa bahati mbaya, baadhi ya *ma-Du'aat* wamezoea kuwalaumu maadui kwa kila balaa na dhulma. Licha ya kwamba mwendo huu unakhalifiana na manhaj iliyo na utakatifu na uongofu ulio wazi wa ki-Utume, lakini ndani yake muna matokeo maovu yenye kusababisha idadi ya mitazamo hasi (*negative attitude*), miongoni mwao yakiwemo:

1. Inakhalifu Kitabu na Sunnah katika taaluma ya uchambuzi wa hali yetu ya leo ya kimaisha ilivyo, kwani Allaah – Aliyetukuka – alizielekeza lawama kwa kushindwa katika vita vya Uhud na Hunayn juu ya Waislamu wenyewe – hata kama ni makafiri ndio walioyafanya ya kufanywa. "Na Mwenyezi Mungu alikukamilishieni miadi yake (yakuwa mtawashinda). Basi mkawauwa kwa idhini yake. Mpaka mliporegea na mkagombana katika shauri lile na mkaasi baada ya yeye kukuonyesheni mliyoyapenda; (hapo ndipo alipoacha kukunusuruni)." [9] Na: "Na siku ya Hunayn (pia); ambapo wingi wenu ulikupandisheni kichwa, lakini haukukufaeni chochote." [10]
2. Katika nyoyo za Waislamu kunapatikana makadirio ya kupita kiasi ya makafiri au kuwathamini mno – jambo ambalo ni lenye kuwazidishia unyonge Waislamu.

3. Ndani yake muna azimio la utakaso wa ubinafsi. Kwa vile inaonyesha yakwamba sisi tushatekeleza yaliyowajibika juu yetu na kustahiki ushindi, na kwamba hatuna tungojealo isipokuwa ni kupewa madaraka juu ya ardhi hii – ingawaje makafiri ndiwo wenye kutushinda. Kwa mitazamo hasi kama hivyo, sisi hatutojali kulea nafsi zetu kwa wema, na kuzihasibu – kama ambavyo itakavyotupelekea kwenye msimamo mwengine wa makosa – nao ni:
4. Kuwa na shaka yakwamba Mwenyezi Mungu Ameshindwa kuweka ahadi yake ya kuwapa Waislamu ushindi, na kwamba makafiri wamezishinda amri za Mwenyezi Mungu, hata kama Mwenyezi Mungu – Aliyetukuka – amesema: "Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo kweli. Na nani mkweli zaidi kwa usemi kuliko Mwenyezi Mungu?" [11]
5. Hili ni suala lenye kuchipuka kutoka katika uchache wa yaqeen (uhakika wa Eemaan) kwa Mwenyezi Mungu, na udhaifu wa kuwa na tawakkul (kujitegemeza) Kwake. Na ukweli yakwamba lawama za yaliyowasibu Waislamu zimetokana na wao wenyewe haimaanishi ati ndio hatuwalaumu makafiri kwa chochote juu ya jinsi wanavyowafanya Waislamu – kwani hili ni jambo tafauti na lile. Mwenyezi Mungu, Mtukufu, Aliye juu - alipotupasha habari kuhusu sababu zilizochangia katika kushindwa vita vya Uhud haikumaanisha yakwamba Allaah amewaondolea lawama kwa yale waliyowafanyia Waislamu." [12]

Kwahivyo, siyasa ya kihakika ni kuitambua nafsi yako mwenyewe; uyatazame mas-ala ya Ummah, na kwamba uyafahamu kihakika matukio ya mazingira yako, kwa kuwalingania watu pamoja na wale walio karibu yako. Na chochote kinyume cha hayo ni mambo ya urongo, upuzi, domo-kaya na kuandama *Hawaa* za nafsi zao – kwani huko ni kwenda kinyume cha uongofu tulioekewa na Mola wa mbingu, na kwenda kinyume na manhaj ya mitume, na kupotea mbali na njia iliyoandamwa na walinganizi walio juu ua njia ya uongofu. Hatahivyo, kuhusu wale wenye kutweta na kuhema, hushtuka baada ya kusakama kwenye Siyasa tupu na wingu la vumbi lilofichika nyuma ya matukio ya kilimwengu – ambayo kwa hakika huoni jipya isipokuwa ni hayo kwa hayo – basi huu ndio mtego tuliowekewa na maadui wa Ummah huu ili waweze kuwapoteza vijana wa ki-Islamu kutoka kwenye msimamo wao ya kihakika, na kuwapoteza kutoka katika maadili ya wajibu wao, na kuwatenganisha na msingi wa mwanzo wa malengo yao.

Hukmu kuhusu Siyasa:

Kutokamana na yale waliyoafikiana nayo Wanavyuoni na yaliyo dhahiri kwa wanafunzi wa ki-ilimu, ni kwamba 'Ilmu ya ki-Islamu na waajib wa ki-Sheri'ah ina vigawanyo viwili, navyo ni (i) Fardh 'Ayn (wajibu wa kila mmoja), na (ii) Fardh Kifaayah (wajibu wa Ummah).

Shaiykh-ul-Islam Ibn Taymiyyah (k. 728) (*rahimahullaah*) amesema: Hapana shaka yakwamba ni waajib juu ya kila mmoja kuamini kwa ujumla juu ya yale aliyokuja nayo Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*). Vilevile, hapana shaka yakwamba kuyajua ki-ukamilifu yote ambayo aliyokuja nayo Mtume (*Sallallaahu 'alayhi wasallam*) ni fardh-al-kifâyah (wajibu wa Ummah) – (yaani; iwapo uwajibu huwo utatekelezwa na kipote cha watu, basi itawatosheleza watu wengine). Kwa vile haya ni mambo yenye kulingana na kuitafakari Qur'aan, kuifahamu na kuizingatia, kuwa na 'Ilmu ya Kitabu na *Hikmah* na kuyahifadhi mafunzo yake, na kulingania katika njia ya Mola juu ya *Hikmah*, mawaidha mazuri, na kujadiliana kwenye njia za uadilifu; na mas-ala mengine mfano wa hayo, ambayo Mwenyezi Mungu aliyafaradhia juu ya Waumini – basi hayo ni miongoni mwa fardh-al-kifâyah (wajibu wa Ummah) juu yao.

Amma kuhusu yale ambayo ni waajib juu ya kila mmoja, basi jambo hili litatafautiana kulingana na uwezekano tafauti, ufahamu na mahitaji, na yale yaliyowapasa kutekeleza kila mmoja wao. Sasa, yaliyo waajib juu ya yule ambae uwezo wake katika kuisikiza ilimu (Qur'aan na Sunnah) , si waajib juu ya asiekuwa na uwezo huo. Vilevile, yaliyo waajib juu ya yule ayasikizae maandiko (Qur'aan na Sunnah) na akayafahamu – kuhusiana na 'Ilmu kwa ufafanuzi – si waajib ju ya yule ambae hakuisikiya hiyo 'Ilmu kwa ufafanuzi. Na pia Mufti (Hakimu wa ki-sheriya katika mahkama), Muhaddith (Mwanachuoni wa Hadeeth), na mdahili (debater) wanawajibika haliyakuwa wasiokuwa wao haitowalazimu. [13]

Mimi nasema: Kwani wewe huoni – Ewe ndugu yangu Muislamu – mpangilio huu wa kita'alamu na ki-Sheriya? Hichi kigawanyo cha Fiqhul-Waaqi' (kuyafahamu malimwengu) kulingana na maadili yake ya kisheriya kinaingia upande gani kwenye mipangilio hii? – wala simaanishi mipango ya kubuni (isiyokuwa na misingi). Kwa kweli hapawezekani kuwa na shaka yoyote kwa yule mwenye kuwa na fahamu za utambuzi yakuwa 'Ilmu ya Malimwengu inawalazimu baadhi ya watu tu katika Ummah huu, ambao huyadhihirisha – kwenye zama tafauti – yenye ukweli yanayodhihirika kwao; kama matokeo ya uchunguzi wao na kuwa waangalifu kwao juu ya yale yenye kuenezwa (au kutangazwa) dhidi ya Waislamu na maadui wa Uislamu, ili wawe chonjo na kuwaonya Waislamu – na wala sio kuchochea hamasa za fujo, wala kuwakatizia watu matumaini.

Hivyo-basi, ni lazima wale waliozama katika 'Ilmu hii wawe waangalifu sana na uhodari wa kupambanua, ili wasiviringwe na kuhadaiwa kutokana na uvumi wa urongo wa watu wenye madaraka, wala habari za uvumi zenye kuenezwa na walaghai. Wala wasiwe kama watoto wadogo wenye kuimbishwa bila ya kujua au kutambua na wakawa hawana uwezo wala fahamu za kuyafanya hayo, kama walivyotekwa akili wengi wa wale

walijishughulisha na somo hili la Fiqh-ul-Waaqi' siku hizi. Na jambo la kushangaza lililojitokeza katika Fiqh-ul-Waaqi' kwenye zama zetu hizi, ni kuwa hapana shaka yoyote yakwamba hakuna mafungamano yoyote katika mnasaba wake na manhaj iliyosawa ya Uislamu.

Ukweli wa mambo ni kwamba, upinzani mkali unaofanywa na walinganizi wa kitagaa hiki cha ilimu wanaoukariri mara kwa mara dhidi ya wasiokuwa wao miongoni mwa Wanavyuoni na wanafunzi wao – hauna uadilifu wala ukweli wowote. Kisha walinganizi hao hudai yakwamba ati wao ndio wenye ilimu zaidi kuhusiana na ufahamu wa malimwengu, na kwamba wao ndio wenye kuzifahamu hali za Mashariki na Magharibi, na kwamba wao ndio wajuzi wa mipangilio ya kiSiyasa na kwahivyo, wao ndiwo wasimamizi wa majukumu haya ya *Fardh-ul-kifaayah* (wajibu wa Ummah wenye kutekelezwa na baadhi, na kuwaruhusu baadhi nyengine wasitekeleze wajibu huu). Sasa ikiwa hali ni kama hii, ni kwa nini wao kuwalaumu wale wasioshiriki?! "Muna nini nyinyi haswa? Mwahukumu vipi mambo?" [14]

Kwahivyo, wajibu wa kisheriya ni kwamba baadhi ya wale wenye kuwa na uwezo wa ufahamu na waisome hali ya malimwengu na wawe ni wenye kuyafuatilia, lakini iwe ni baada ya kuwa na 'Ilmu muafaka yenye ufafanuzi wa Shariya yenye kudhihirika ukweli wake yakiandamana na tahadhari tafauti zilizotakasika – ili msingi wa mas-ala yenye utatanishi uweze kupambanuliwa na mambo yasiwe na utatanishi.

Kisha sisi twasema kuhusu madai ambapo baadhi ya hawa walinganizi huwafutilia mbali na kuwang'oa wengine – kutokana na 'ujinga wao wa mas-ala ya kilimwengu', au 'kutojali kwao na kutojishughulisha na Ummah pamoja na njama zilizopangwa dhidi yake', kwa hakika, mara nyingi madai hayo yana udhalimu na urongo, na yako mbali na ukweli wa mambo ulivyo. Kwani, ni kwa vipimo gani waliupima uangalifu huu, au walipima kwa vipimo gain ufahamu wa mtu kuhusu mambo ya kilimwengu? Yote hayo ameyaegemeza juu ya baadhi ya udondozi wa aliyoyasema mtu fulani, au baadhi ya khutbah zilizotolewa, au baada ya kukusanya magazeti na majarida, Ah! Huu ni ukosefu wa adabu na upotofu ulioje!

Kwa hakika kuteseka bila ya kuhurumiwa, kuwa muangalifu na kujitahidi na kufanya juhudi kwa utulivu kuhusiana na ufahamu wa sehemu yoyote ya Wahyi Mtukufu (yaani; Qur'aan na Sunnah) ni mara elfu-moja bora kuliko makelele ya waenezao uvumi, na majigambo ya wenye kujinaki, na kijiita 'watu wa fikra' – ambazo, nyingi, zimejengwa juu ya kudhaniwa, Kubahatisha, na makisio yaliyo hafifu!!

Amma kweli, Simba wanyonge ndiwo wangurumao kwa nguvu, na wenye nguvu hawana haja ya kujidai, wala kudanganya.

Kumbukumbu:

1. Kutoka katika Fiqhul-Wâqi' baynan-Nadhariyyah wat-Tatbîq (uk. 28-37) .

2. Imepokewa na al-Bukhârî (6/360) na Muslim (uk. 1842)

3. Linganisha haya na Khatat (3/357) cha al-Maqrîzî (k.845H)

4. Hiki ni kitabu kilichoandikwa na Mtaliani aitwae, Niccolo Machiavelli (k.940H/1532CE).

5. Kutoka kwenye maneno ya Shaykhul-Islâm Ibn Taymiyyah kutoka kwenye kitabu chake kiitwacho, "Siyâsatush-Shar'iyyah" (uk. 11).

6. al-Jamâ'âtul-Islâmiyyah fî Daw'il-Kitâb was-Sunnah (uk. 166) of Shaykh Salîm al-Hilâlî.

7. Sûratush-Shûrâ 42:30

8. Sûratun-Nisâ' 4:111

9. Sûrah Âli-'Imrân 3:152

10. Sûratut-Tawbah 9:25

11. Sûratun-Nisâ' 4:122

12. as-Sabîl ilâ Manhaj Ahlus-Sunnah wal-Jamâ'ah (uk. 38-39)

13. Majmû'ul-Fatâwâ (3/312)

14. Sûrah Yûnus 10:35